SWAHILI FORUM XI (2004): 107-119

MASUALA YA KISARUFI KATIKA MAGAZETI YA MITAANI YA KISWAHILI – TANZANIA

YARED M. KIHORE

1. Utangulizi

Baada ya kupitishwa kwa sheria iliyoruhusu kuanzishwa kwa magazeti binafsi mnamo 1992, kumeibuka magazeti mengi ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania yanayochapishwa kila siku, kila wiki au mara kadha kwa wiki, kwa mwezi, na kadhalika Magazeti kama haya hufikia zaidi ya hamsini nchini humu. Miongoni mwake, kuna yale yanayochukuliwa kuwa "rasmi" kwa maana kwamba yanatoa taarifa rasmi za ndani na nje ya nchi. Taarifa rasmi tunaichukulia hapa kuwa ni ile inayohusu matukio halisi ambayo, kwa kawaida, huwa pia yanahusishwa na mamlaka au chanzo fulani maalumu na kutolewa kwa namna na katika mazingira rasmi. Hapa, namna na mazingira rasmi ya kutolewa habari husika ni yale yanayoendana na kaida katika jamii, kisheria na kiutamaduni. Magazeti katika kundi hili yana majina jumuishi kama vile "Mtanzania", "Majira", "Mwananchi", "Rai", "An-nuur", na kadhalika.

Kundi jingine la magazeti haya ni lile linalojihusisha na taarifa za michezo. Taarifa za michezo ndani ya magazeti haya nayo, kwa kiasi kikubwa, ni rasmi kwa kuwa ni matukio halisi yaliyoshuhudiwa na waandishi au kupatikana kutokana na vyanzo fulani vya hakika. Magazeti katika kundi hili yana majina ya kimichezo au ya kiburudani moja kwa moja, kama vile "Dimba", "Mwanaspoti", "Lete Raha", na kadhalika.

Aidha kundi jingine ni lile la magazeti yanayojulikana kwa jumla kama "Magazeti ya Mitaani". Magazeti katika kundi hili yanabeba mada nyingi mbalimbali zinazohusu mambo ya watu mitaani, masuala ya mambo ya kidini mitaani, vichekesho, na mara nyingi yale yanayowasibu wanajamii mitaani mmojammoja au kwa jumla. Hapa tunatumia neno "mitaani" kwa maana ya maeneo ya mijini wanakoishi watu, ambayo katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981: 192) huitwa "viambo" au "vitongoji". Na, kwa hakika, mambo mengi yanayoelezwa katika magazeti kwenye kundi hili yanahusu zaidi vituko, visa na vitimbi vya watu katika maeneo haya kama tulivyogusia hapo juu. Kwa kawaida, haya si mambo yanayoaminika au kupokelewa moja kwa moja au kwa urahisi na kila mtu. Kutokana na hali hiyo huwa hayachukuliwi kama taarifa rasmi. Lakini, kwa kiasi kikubwa pia, lugha inayotumiwa humu ni ile isiyokuwa rasmi kwa maana kwamba kama ni maneno au misemo, basi mengi si yale yaliyokwishaidhinishwa na vyombo rasmi au ambayo matumizi yake hadharani hayapokelewi na wasomaji wote kwa namna chanya (taz. dhana ya *Kiswahili cha Mitaani* katika Blommaert 1990: 22-29). Katika kundi hili tunapata magazeti yenye majina kama "Kasheshe", "Kombora",

“Msema Kweli”, “Nyakati”, “Uwazi”, “Maisha”, na kadhalika Hapa bila shaka baadhi ya wasomaji watashangaa ni kwa nini hata magazeti yaliyojitaja wazi kuwa ni ya “Kikristo” kama *Msema Kweli* na *Nyakati* nayo tumeyaweka katika kundi hili. Jambo hili litaelezwa katika sehemu inayofuata.

Kundi la nne ni la magazeti yanayotoka mchana jijini Dar es Salaam. Katika kundi hili yapo magazeti mawili tu ambayo ni *Alasiri* na *Darleo*. Magazeti haya kila moja yaonekana kuandika habari rasmi na habari za mitaani kama tulivyozifafanua hapo juu. Kwa kuwa nchini Tanzania, tofauti na nchi nyingine kama vile nchi za Ulaya, magazeti yote yamekuwa yakianza kuuzwa asubuhi, inaelekea magazeti haya yalianza kutolewa mchana kufuata mifano katika nchi hizo na/au kujaza hilo pengo la kutokuwepo magazeti yanayoanza kuuzwa mchana. Haya, kwa kawaida, hutangaza matukio yaliyotokea baada ya magazeti yaliyotoka asubuhi. Baadhi ya matukio kama hayo ndiyo pia huingia katika magazeti ya siku inayofuata.

Nia yetu katika makala haya ni kuchunguza masuala ya kisarufi katika maelezo yanayojitokeza katika magazeti ya hilo kundi la tatu, yaani, magazeti yanayojulikana kwa wananchi wengi nchini Tanzania kama “magazeti ya mitaani” kwa maana tuliyoitoa katika aya iliyotangulia. Tunafikiri pia kuwa inafaa katika hatua hii tueleze tunachokikusudia tukisema “masuala ya kisarufi” ambayo tuna nia ya kuyachunguza.

Kwa kiasi kikubwa, masuala ya kisarufi yatakuwa ni mambo yanayohusu maneno yaani msamiati na misemo inayotumiwa na magazeti haya, miundo ya sentensi zinazohusika na matumizi mengine ya lugha kwa jumla katika magazeti haya. Ni dhahiri kuwa magazeti haya yanasomwa sana na wananchi wa kawaida mitaani. Hawa inawezekana wanapenda kuyasoma kwa sababu mbalimbali kama vile mada zilizomo, lugha iliyotumika humo, na kadhalika. Lakini cha muhimu zaidi kwetu ni kujua maumbile ya jumla ya lugha hiyo na pengine kama ndiyo chanzo cha kupendwa kwa magazeti haya na wasomaji wengi. Tutachunguza masuala haya kwa utaratibu ufuatao. Kwanza tutachunguza kwa undani sifa za jumla na mahsusi za magazeti haya katika sehemu inayofuata. Baada ya hapo tutatazama lugha inayotumiwa katika magazeti hayo ili tuweze kubainisha masuala ya kisarufi ambayo tunakusudia kuyachunguza. Kisha tutatoa hitimisho.

Mbinu ya utafiti iliyotumika ni ile ya kukusanya nakala kadha wa kadha za magazeti 13 tuliyoyaweka katika kundi hili, kuchunguza namna zake mbalimbali za kutoa taarifa na kisha kuchanganua masuala ya kisarufi katika taarifa hizo. Magazeti yaliyokusanywa na kuchunguzwa ni *Kasheshe*, *Kombora*, *Uwazi*, *Macho*, *Amani*, *Komesha*, *Ijumaa*, *Maisha*, *Cheka*, *Nyakati*, *Msema Kweli* na *Buzuki*.[1]

[1] Gazeti la kumi na tatu lililochunguzwa ni *Michapo,* lakini katika makala zake nyingi linatumia lugha rasmi.

2. Sifa za magazeti ya mitaani

Ingawa tumekwishataja baadhi ya sifa za jumla za magazeti ya mitaani katika sehemu iliyotangulia, tunafikiri ni muhimu katika hatua hii kuchunguza sifa zote za magazeti haya kwa undani zaidi. Ili kuweka mtiririko mzuri tutagawanya sifa hizo katika makundi mawili, yaani, kundi la sifa za jumla na lile la sifa mahsusi.

2.1. Sifa za Jumla za Magazeti ya Mitaani

Kama tulivyodokeza katika sehemu ya kwanza hapo juu, sifa ya jumla kabisa ya magazeti haya ni aina za mada zilizomo ndani yake na jinsi zinavyoelezwa. Tungependa suala la aina za mada na jinsi zinavyoelezwa vitazamwe pamoja kwa sababu mambo haya mawili yanaonekana kuwa yanafungana sana. Katika utangulizi hapo juu tulidokeza kwa jumla kuwa magazeti haya, kwa kiasi kikubwa, huwa yanaeleza vituko, visa na vitimbi ambavyo hata watoaji wake huwa wanajua kuwa vinaweza kuwaweka wasomaji katika hali isiyokuwa ya kawaida. Matokeo au athari ya mada hizi hudhihirika, mathalani, katika maelezo yanayotumiwa kutangaza gazeti la *Kasheshe* radioni kila wiki. Maelezo hayo katika tangazo hilo huwa yanamalizika kwa maneno "[...] na wala usisite kulisoma [= gazeti la *Kasheshe*] mbele ya wanao". Hii ina maana kwamba magazeti haya yamekuwa yakibeba mambo ambayo hayastahili kusomwa na watoto au na wazazi mbele ya watoto wao. Na kama tutakavyoonyesha mwishoni mwa kijisehemu hiki, mada hizo na jinsi zinavyoelezwa ndivyo vimekuwa msingi wa mgawanyiko baina ya wasomaji wa magazeti nchini Tanzania.

Kabla ya kueleza sifa nyingine za jumla za mada zinazojadiliwa katika magazeti haya hebu tupate mifano michache ya mambo yanayojadiliwa kwa kukariri baadhi ya mada zilizojitokeza katika kurasa za mwanzo za baadhi ya magazeti hayo:

1. (a) "Hii ni Aibu kubwa! Mabinti wa kigogo wamwaga picha za X mitaani" (*Kombora,* Mei 19-25, 2003)
   (b) "Mtambo mwingine wa kutolea mimba wagundulika jijini Dar" (*Kombora*, Mei 19-25, 2003)
   (c) "Rais Mkapa Upoo? (*Uwazi,* Mei 20-26, 2003)
   (d) "Pasua Jipu: Nachukia Wawekezaji wezi" (*Uwazi,* Mei 20-26, 2003)
   (e) "Masikini Dk. Remmy: Aikimbia familia yake" (*Macho,* Mei 22-28, 2003)
   (f) "Apigwa mande eti akilinda hadhi yake" (*Macho,* Mei 22-28, 2003)
   (g) "Sista Asha: Mahaba yakichombezwa na mambo f'lani mapenzi yatadumu" (*Amani,* Mei 22-28, 2003)
   (h) "Tahadhari: Machangudoa wana vidonge vya usingizi" (*Komesha,* Mei 24-30, 2003)

(i) “Ajifungua paka kutokana na mimba ya miezi 120” (*Komesha,* Mei 24-30, 2003)

(j) “Mao Santiago ni mwanaume kama binti? Yadaiwa yeye, Wakongo kibao ‘wameolewa’ na mijimama” (*Kasheshe,* Machi 26-Aprili 1, 2003)

(k) “Waislamu Dar wachangamkia ‘kiti moto’ baada ya Sheikh kuipiga marufuku” (*Msema Kweli,* Mei 18-24, 2003)

Katika (1), tumekariri baadhi tu ya mada zinazojitokeza katika kurasa za mwanzo za baadhi ya magazeti ya mitaani. Sifa ya kwanza inayodhihirika katika mada hizo ni kwamba zote humfanya msomaji akishangae kile kinachotajwa. Hii ni kweli kwa magazeti yote ya mitaani ikiwemo hata lile la “Kikristo” katika (1k). Hali hii ya kukishangaa kile kilichotajwa katika mada ndiyo ama hufanya baadhi ya watu kukosa hamu hata ya kufikiria kununua magazeti haya au huwachochea watu wengine kufanya kila juhudi kuyapata magazeti hayo. Sifa ya pili inayodhihirika ni kuwa hata kama mada haishangazi, namna maelezo yanavyofanywa gazetini kuhusu mada huweza kumfanya mtu ajiulize kama kinachosemwa ni cha kweli au cha kubuni tu. Kuna baadhi ya watu ambao wanadai kwamba pamoja na maelezo hayo kuwa ya ajabuajabu, bado mengi ni matukio ya kweli na kwamba hayakubuniwa tu. Kama tulivyodokeza mwanzoni mwa kijisehemu hiki, sifa hii ya pili pia ndiyo imekuwa msingi mkubwa wa tofauti za kimtazamo baina ya wasomaji wa magazeti nchini Tanzania. Kwani wakati wengine wakipendelea “ukweli” utolewe hadharani bila wasiwasi, wengine wanafikiri kwamba maelezo katika magazeti haya, hata kama ni ya kweli, si vizuri “yamwagwe ovyo” hadharani, kwa maana kwamba yasisambazwe na kufikishwa hata kusipohusika.

Sifa ya tatu inayojitokeza hata katika hizo mada chache zilizokaririwa ni aina ya msamiati na misemo ambayo, kwa kawaida, haijitokezi katika magazeti rasmi. Maneno kama “mande” (1f), “chombeza” (1g), “machangudoa” (1h), “mijimama” (1j) na “kiti moto” (1k) hayapatikani katika kamusi sanifu. Vilevile misemo kama “mwaga picha” (1a), “linda hadhi” (1f), “changamkia” (1k), na kadhalika haina maana za kawaida katika mazingira yalimotumika. Kwa mfano, “anayelinda hadhi” katika (1f), hakika ni kwamba amezidi kuharibu mambo kwa msingi wa yale yanayosimuliwa katika maelezo. Vivyohivyo, “kuchangamkia” kitu kilichopigwa marufuku na ambacho hakiruhusiwi kwa misingi ya dini, si kawaida. Maneno na misemo hii imetokana zaidi na mazungumzo ya kawaida mitaani. Kinachoshangaza ni vituko, visa na vitimbi vinavyoihusisha. Kwa mfano, wakati “kiti moto” ni lugha ya kawaida ya mitaani jijini Dar es Salaam kwa maana ya nyama ya nguruwe ya kuchoma, matumizi yanayoihusisha na Waislamu ambao misingi ya dini yao haiwaruhusu kutumia nyama hiyo ndicho kioja. Na, jinsi hii ya kutumia lugha ya mitaani katika visa mbalimbali katika magazeti hayo ndiyo imefanya tuyaweke magazeti fulani yaliyojitaja wazi kuwa ni ya “Kikristo” katika kundi la magazeti ya mitaani. Kwa maoni yetu, lugha kama hii haijitokezi katika gazeti kama *An-nuur* ambalo pia ni la kidini. Hadi sasa tunachojua ni kuwa kitu ambacho hakipendelewi na baadhi ya watu kwenye magazeti haya

ni mada kama ilivyoelezwa katika aya iliyotangulia. Hatujajua ni kwa kiasi gani lugha pia huchangia katika kupendwa au kutopendwa kwa magazeti haya.

Sifa ya nne ya jumla ya magazeti haya ni kuhusu uchapishaji wake. Idadi kubwa ya magazeti haya huchapishwa na walewale wanaochapisha magazeti rasmi. Yaonekana kutokana na kununuliwa kwa wingi kwa magazeti haya na wananchi wa kawaida, wachapishaji wengi wanayachapisha kama njia ya kujipatia au kujiongezea kipato. Hali hii pia imefanya uandishi "urekebishwe" (taz. tangazo la *Kasheshe* lililotajwa katika (1j) hapo juu) kwa kiasi fulani katika magazeti haya ili yasijikute yakipigwa marufuku na serikali kama ilivyowahi kufanyika huko nyuma kwa baadhi ya magazeti. Marekebisho hayo pia husaidia kuwavutia wasomaji zaidi.

2.2. Sifa Mahsusi za Magazeti ya Mitaani

Miongoni mwa mambo tunayoweza kuyataja kama sifa mahsusi ya magazeti ya mitaani ni kujihusisha kwake zaidi na mambo binafsi ya mtu au ya makundi ya watu. Sehemu kubwa ya mambo yanayoelezwa katika magazeti haya ni visa, vituko, vitimbi, na kadhalika vya watu, hasa watu maarufu katika jamii kwa mabaya au kwa mazuri. Magazeti haya pia kwa viwango mbalimbali yamesukuma sana mbele sanaa ya vibonzo au makatuni na vilevile matumizi ya picha kwa jumla.

Aidha, sifa nyingine tunayofikiri kuwa ni mahsusi kwa magazeti haya ni uhuru wa kutumia lugha ya Kiingereza moja kwa moja au kama maneno ya mkopo kutoka katika lugha hiyo. Hebu tazama hii mifano katika (2):

2. (a) "Mashoga watwangana kwenye Kitchen Party" (*Cheka*, Mei 24-30, 2003)
   (b) "Nusura mwanamuziki aibiwe gesti... akamtaimu changu na kumgeuzia kibao" (*Komesha*, Mei 24-30, 2003)
   (c) "Only God Can" Amani (katika jina la gazeti la *Amani*)[2]
   (d) "The story from Nigerian Movies" (Kichwa tu, *Amani*, Mei 22-28, 2003)
   (e) "Why did you kill me Patricia? (Kichwa tu, *Ijumaa*, Mei 23-29, 2003)
   (f) "diet for ENGLISH readers" (Makala nzima, *Nyakati*, Mei 18-24, 2003)

Katika (2), tunaona mifano mbalimbali ya maneno au tungo za Kiingereza ambazo zinajitokeza katika baadhi ya magazeti ya mitaani. Hii hujitokeza kama maneno kama katika (2a) na (2b), kama vichwa vya habari tu kama katika (2c-2e) na kama kichwa na habari nzima kwa Kiingereza kama katika (2f). Blommaert (keshatajwa: 24) anaeleza "Kiswahili cha Mitaani" kama "vilugha vya Kiswahili vilivyoingiliwa na Kiingereza vitumiwavyo katika maeneo ya mijini nchini Tanzania". Blommaert anaeleza zaidi kuwa vilugha hivi ni vya burudani vinavyotumiwa sana na

[2] Maneno hayo ya Kiingereza yanawekwa juu ya jina la gazeti "Amani" ukurasa wa nje. Maneno hayo yanatumiwa zaidi kama sehemu ya jina la gazeti.

vijana na vyenye kuonyesha kupendelewa kwa Kiingereza cha Kimarekani. Kwa hiyo, hii inazidi kuthibitisha kuwa lugha ya kwenye magazeti haya nayo ni lugha ya mitaani. Uwezekano kuwa ama wapenzi au wenye magazeti wanapendelea Kiingereza hudhihirika katika mifano kama hiyo tuliyoitoa katika (2), lakini mbali na matumizi kama vile ya "taimu" kama kitenzi katika (2b), hatukuona mifano mingi ya aina alizozikariri Blommaert (keshatajwa) kama vile "no swet dali, I rav you", "unajipraudipraudi", na kadhalika Licha ya matumizi mbalimbali ya maneno ya Kiingereza kama ilivyotajwa, inaonekana kama kuna Kiswahili kingine cha mitaani ambacho kinaelekea kutofautiana na hicho cha vijana kilichochunguzwa na Blommaert na ambacho hivi sasa kinakuzwa kiandishi. Lakini inawezekana pia kuwa katika mazingira haya mbalimbali, maelezo ya Kiingereza yanatolewa zaidi kama njia ya kuweka kumbukumbu halisi ya matukio, vituko na vitimbi katika jamii na wanajamii. Hii ina maana kwamba kama maelezo yanamhusu mtu aliyekuwa akichanganya lugha ya Kiingereza, basi hayo maelezo yake yanatolewa yalivyo. Hii inatufikisha katika haja ya kutazama, katika sehemu inayofuata, maumbile mbalimbali ya lugha katika magazeti ya mitaani.

3. Lugha katika magazeti ya mitaani

Baada ya kuchunguza sifa mbalimbali za magazeti ya mitaani, sasa tungependa tuchunguze kwa undani maumbile ya lugha inayotumika humo. Tumeona katika sehemu iliyotangulia kuwa yale yanayoelezwa katika magazeti ya mitaani, huelezwa pia, kwa kiasi kikubwa, kwa Kiswahili cha mitaani. Lakini Kiswahili hiki cha mitaani kimeonekana ni jumla ya vilugha mbalimbali vinvyotumiwa katika maeneo ya mijini ambavyo sifa zake hazijachunguzwa kwa ukamilifu. Aidha hapo awali vilugha hivyo vilikuwa vikizungumzwa tu na wahusika. Lakini sasa hivi vilugha hivyo vimejitokeza katika maandishi kwenye magazeti ambayo yanazidi kuwa maarufu. Sasa cha kuuliza ni je, katika maandishi kwenye magazeti ya mitaani, bado vilugha hivi vinajitokeza kama vilugha vingivingi vya Kiswahili au kama kilugha kimoja kiandishi?. Je, vilugha au kilugha hicho kina maumbile gani ya kisarufi?

Katika sehemu hii tutachunguza masuala ya kisarufi ya lugha katika magazeti ya mitaani. Kama tulivyogusia katika utangulizi, masuala hayo yatahusu maneno yaani msamiati, misemo na tungo mbalimbali katika magazeti hayo nia ikiwa ni kubainisha sifa au maumbile maalumu ya lugha inayotumika humo. Tutaanza kwa kutazama kwa ufupi tu maendeleo ya nadharia za kiisimu katika kukabiliana na uchunguzi wa namna hii. Baada ya hapo tutatazama masuala yanayohusiana na maneno yaani msamiati na misemo katika lugha ya magazeti ya mitaani; na kisha masuala kuhusiana na tungo mbalimbali.

3.1 Maendeleo katika Nadharia za Kiisimu

Uchunguzi kama ule wa Blommaert (keshatajwa) tuliourejea hapo juu kuhusiana na kuwepo kwa vilugha vinavyojulikana kama Kiswahili cha Mitaani ulikitwa katika misingi ya Isimujamii. Misingi ya kiisimujamii, kama ilivyo kwa upande wa isimu anthropolojia, inaonekana kukosa

mkabala unaozingatia mitazamo ya wenyeji wa lugha na vilevile ya uchunguzi wa lugha katika muktadha wake wa kijamii na kiutamaduni (Palmer 1996: 35). Kwa mfano, katika uchunguzi wa Blommaert na wenzake waliomtangulia, kilichosisitizwa kuhusiana na matumizi ya maneno ya Kiingereza katika lugha ya mitaani ni mapenzi ya watu kwa lugha hiyo kwa lengo la kujibainisha kama kundi maalumu lenye hadhi fulani. Lakini mchunguzi huyo anaona pia kuwa hii, kwa kiasi fulani, ilisuluhisha tatizo la mgogoro kuhusu hadhi ya Kiswahili au Kiingereza katika Tanzania ya Kijamaa (keshatajwa: 24). Hizi, kwa kiasi kikubwa, ni tafsiri za wachunguzi na haidhihiriki ni kwa kiasi gani zilikuwa pia mitazamo ya wachunguzwa. Kutokana na mapungufu ya mikabala kama hii ndiyo kukaibuka mkabala wa kinadharia unaojulikana kama **Isimuutamaduni** yenye misingi ya mbinu za ushawishi uliodhibitiwa, uchunguzi wa mshiriki na maelezo ya kiethnografia katika miktadha asilia. Kwa kifupi, mkabala huu wa kinadharia unahusisha vilugha vya kiisimu na kaida za mawasiliano kama zinavyoongozwa na vielelezo vya kiisimujamii (Palmer, keshatajwa: 36). Mkabala wa aina hii ungekuwa wa manufaa zaidi katika uchunguzi wa Kiswahili cha mitaani. Tunachukulia uchunguzi wetu wa lugha katika magazeti ya mitaani kama hatua kuelekea katika uchunguzi wa Kiswahili cha Mitaani uliokitwa katika misingi ya Isimuutamaduni.

3.2 Maneno yaani Msamiati na Misemo katika Magazeti ya Mitaani

Kama tulivyoona katika mifano katika (1) na (2) hapo juu, maneno yanayotumiwa katika magazeti ya mitaani ni ya aina tatu: yale ya kawaida yanayopatikana katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, yale ya mitaani ambayo hayamo au hayajaingia katika kamusi sanifu na yale yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiingereza. Hapa hatutajihusisha na maneno ya kawaida yaliyomo katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Tutajihusisha zaidi na maneno ya mitaani na kwa kiasi fulani yale yaliyokopwa kutoka katika lugha ya Kiingereza. Kwa kuwa kundi hili la nyuma lilikwishagusiwa katika sehemu zilizotangulia, tunafikiri ni muhimu tuanze nalo na kisha turejee kwenye kundi la maneno na misemo ya mitaani.

3.2.1 Maneno yaliyokopwa kutoka Kiingereza

Ukiacha kando maneno ya Kiingereza yaliyotumiwa moja kwa moja katika vichwa vya habari au katika maelezo, magazeti haya hutumia pia maneno ya mikopo kutoka katika lugha hiyo kama inavyojitokeza katika (3) hapa chini:

3. (a) “Nesi Magreth alimwambia dokta Frank ambaye alikuwa bize na shughuli ya kumpima mgonjwa.” (*Ijumaa*, Mei 23-30, 2003, uk. 2)
   (b) “Chache kati ya nyingi zikiwa ni mapozi yake...” (*Ijumaa*, iliyokaririwa, uk. 3)
   (c) “Eti Promota anabeep” (*Amani*, Mei 22-28, 2003, uk. 6)

Katika (3), tunaona mifano ya maneno yaliyokopwa kutoka katika Kiingereza. Maneno haya yanajitokeza katika maumbile mawili. Umbile la kwanza ni lile linaloonyesha matamshi ya

Kiingereza kama katika (3a-3b); na la pili ni lile linaloonyesha maandishi ya lugha hiyo kama katika (3c). Mifano ya umbile la kwanza inaonyesha kujitokeza zaidi kuliko ile ya umbile la pili. Kwa jumla, japokuwa mikopo hii bado inajitokeza hapa na pale, katika magazeti mengi maneno ya aina hii yamepungua sana katika makala mbalimbali. Unaweza kuhisi kuwa hii ni namna mojawapo ya uboreshaji uliofanyika katika magazeti haya.

Hata hivyo, pamoja na mikopo ya aina hiyo kutoka katika lugha ya Kiingereza, kuna aina nyingine ya matumizi inayoyapa maneno ya Kiswahili sura ya maneno ya Kiingereza. Mfano hapa ni kama huu katika (4):

4. (a) "...kutafuta sana totoz.." (*Macho*, Mei 22-28, 2003, uk. 4)
   (b) "unapokutana na mkeo Gesti ukiwa na 'totoz'" (*Maisha*, Aprili 7-13, 2004)

Hapa shina la neno la Kiswahili "toto" limeongezewa [z] la Kiingereza linaloashiria wingi. Lakini cha muhimu cha kutazama hapa ni kwamba wakati katika (4a) neno hili limetumiwa bila alama yoyote katika (4b) limewekewa alama za mnukuo.

Katika magazeti haya inajitokeza pia namna nyingine ya matumizi ya lugha ya Kiingereza inayotumia vifupisho. Kifupisho kilichojitokeza sana hasa katika gazeti la *Buzuki* ni "a.k.a" ambayo kwa Kiingereza ni "also known as". Hiki hutumika kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

5. (a) "Msanii Castro Marceline, a.k.a. Caz T, si mtu mgeni miongoni mwa .." (*Buzuki*, Mei 19-Juni 2003, uk. 4)
   (b) "Halikadhalika msanii wa luninga Ummy Wenceslaus a.k.a Dokii, ni hivyo hivyo" (*Buzuki*, keshatajwa)
   (c) "Ni ajabu na kweli, Wambura sio jina la baba mzazi wa malkia wa R&B Lady Jay Dee, a.k.a. Jide a.k.a. Mama Some Food, a.k.a. Machozi, a.k.a Wallet, a.k.a. Komando, Buzuki limegundua" (*Buzuki*, keshatajwa, uk. 8)

Kuhusu mfano wa kifupisho katika (5), yafaa ielezwe kwamba hakuna mahali gazetini kunapotolewa ufafanuzi wake. Inaelekea imechukuliwa tu kuwa kwa mpangilio huo wa majina mbalimbali ya wahusika msomaji ataelewa kinachosemwa. Lakini kuna baadhi ya watu waliotafsiri kifupisho hiki kama "au kama anavyojulikana". Cha muhimu hapa ni kwamba kwa kuwa yanafuata majina mengine ya mhusika yanayojulikana kwa watu mitaani, kifupisho hicho kinaweza kuwa cha Kiingereza au cha Kiswahili bila maana ya maelezo kuathirika.

3.2.2 Maneno au Msamiati wa mitaani

Kutokana na matumizi yake kila siku ndani ya magazeti ya mitaani, leo hii kuna maneno au msamiati unaojibainisha moja kwa moja kama maneno ya mitaani. Mifano ya maneno haya ni kama vile:

6. (a) njagu – ‘polisi’
   (b) denti – ‘mwanafunzi msichana’
   (c) kimwana – ‘binti mzuri’
   (d) njemba – ‘mtu mwenye uwezo’
   (e) miwaya – “ukimwi”
   (f) saula – ‘kuvua nguo hadharani’
   (g) bonda – ‘piga’
   (h) kong’ota – ‘piga hasa kwa fimbo’
   (i) tinga – ‘kaa bila nia ya kuondoka'
   (j) tonya – “pasha, dokeza”, na kadhalika

Mifano katika (6) ni ya maneno ya mitaani ambayo ni nomino (6a-6e) na vitenzi (6f-6j). Maneno kama haya ni mengi na tunafikiria kuandaa orodha yake katika kazi itakayofuata. Tungependa tuongeze maelezo hapa kwa kuonyesha kwamba kisarufi, maneno ya mitaani nayo yana aina ya maneno inayojulikana kama vivumishi. Mifano ya vivumishi katika lugha ya mitaani ni kama vile “bomba”, “poa”, na kadhalika ambayo katika lugha ya kawaida ni nomino na kitenzi kwa mfuatano huo. Kitu “bomba” ni kitu kizuri sana na jambo “poa” ni jambo lililotulizana, lisilo na vurugu ya aina yoyote.

Lakini tunaweza pia tukaona mifano zaidi ya maneno haya katika (2) na (3) hapo juu ambayo ni kama vile “mande”, “kitimoto”, “chombeza”, “machangudoa”, “mijimama”, n.k Miongoni mwa maneno haya kuna yale yaliyoundwa tu mitaani si miaka mingi iliyopita k.m. “kitimoto” na “machangudoa” lakini pia yapo yale ambayo yamekuwa yakitumika mitaani kwa muda mrefu ingawa hayajawahi kuingia katika matumizi sanifu, k.v. “mijimama” na “chombeza”. Katika orodha hii neno “chombeza” ni kitenzi na mengine yote yaliyobaki ni nomino.

Kuhusu nomino, pengine ni vizuri tugusie kidogo suala la ngeli zake. Hapa inadhihirika kwamba japokuwa baadhi yake zinatenganishika vizuri katika umoja na wingi (k.m. njagu – manjagu; kimwana – vimwana; denti – madenti, na kadhalika), nyingine hazitenganishiki kwa urahisi namna hiyo. Mifano ya nomino katika kundi hili la nyuma ni ile kama “mijimama”, “misoksi” (*Maisha*, keshatajwa, uk. 2), “miwaya”, na kadhalika, ambayo ni dhahiri iko katika wingi na pengine katika ngeli ya 4, yaani ngeli ya MI-. Hapa swali ni je, nomino hizi zina maumbo katika umoja au la; na kama yapo ni yapi? Kwa mfano, mitaani, mbali na neno “mijimama” kuna maneno “mimama”, “jimama”, na kadhalika.[3] Hapa umbo “jimama” ndilo liko katika umoja. Sasa, je, ndilo umbo la umoja la “mijimama” au la “mimama”? Na kwa jibu lolote litakalotolewa, jozi husika itakuwa katika ngeli gani? Haya ni masuala yanayohitaji kuchunguzwa zaidi.

Kwa jumla maneno kama hayo yaliyoelezwa, kutokana na maana zake mitaani, yanachangia sana katika kuyatilia uzito na mvuto maelezo ya vituko, visa na vitimbi mitaani.

[3] Maneno "mimama" na "mijimama" inatumika kuita wanawake ambao wana taratibu au sura zenye kuonyesha ubabeubabe hivi hasa katika kuendesha shughuli zao mitaani. Mijimama ndio hufanya shughuli hizo kwa ubabe mkubwa kuliko mimama.

Ama kuhusu maneno yanayoambatanishwa tumekumbana na umbo "dadake" (*Kasheshe*, Aprili 7-13, 2004, uk. 7) na vilevile "baba'ake" (*Buzuki*, keshatajwa, uk. 8) au "babaake".

3.2.3 Misemo ya mitaani

Kama ilivyo kuhusiana na msamiati, magazeti ya mitaani nayo yanaonyesha utajiri mkubwa wa misemo ambayo inajibainisha kuwa ni ya mitaani. Katika magazeti haya ni kawaida kukutana mara kwa mara na misemo kama hii katika (7):

7. (a) pata kigugumizi – 'pigwa butwaa na kushindwa kujieleza'
   (b) tembeza bakora – 'piga kwa fimbo ovyoovyo'
   (c) pata mkong'oto – 'pigwa hasa kwa fimbo mara nyinginyingi'
   (d) zua sokomoko – 'anzisha vurugu'
   (e) pewa ujiko – 'kusifiwa'
   (f) chacha vibaya – 'kutokuwa na fedha kabisa'
   (g) jaa ile mbaya – 'kuwa na fedha nyingi'
   (h) shindwa kufurukuta – 'kukosa uwezo wa kujitetea katika ushindani au ugomvi'

Mifano katika (7) ni ya misemo ambayo ni ya kawaida sana ingawaje si ya lugha ya kawaida. Hii ni pamoja na kwamba maneno moja moja yanayoiunda misemo hii ni maneno ya kawaida katika lugha. Sifa ya misemo ya mitaani huonekana pia katika maana zake. Kwa mifano yote katika (7), kila moja ina maana ileile mitaani isipokuwa (7b) iliyo na maana ya pili ya ufanyaji wa ngono kwa mujibu wa matumizi yake huko katika mitaa ya Zanzibar.

Lakini katika magazeti tuliyoyachunguza kuna mifano mingine mingi ya misemo ya mitaani. Hii ni kama vile "kupiga chabo", "kupiga ulabu", "wanaume kama mabinti", "domo-kujaa", kwa maana za "kuzini", "kunywa pombe", "mapenzi kinyume cha maumbile" na "kushindwa kuongea". Orodha kamili ya misemo kama hii nayo inaandaliwa katika kazi itakayofanywa baadaye. Katika sehemu inayofuata tutaona jinsi baadhi ya misemo ya mitaani inavyojitokeza katika tungo mbalimbali.

3.3 Tungo katika magazeti ya mitaani

Pamoja na vichwa vya habari na mada za kushangaza kama tulivyoona katika sehemu zilizotangulia hapo juu, miundo ya sentensi katika magazeti haya inaonekana ni ya kufuata kanuni za kisarufi pengine hata kuliko ilivyo katika magazeti rasmi.Hii inaelekea ni kutokana na mada ambazo ni za mitaani na zenye kuweza kuelezeka vizuri na wahusika au na walio karibu na mazingira hayo. Hebu tuanze kwa kutazama mifano hii ya jumla ya taarifa za kawaida za matukio mitaani:

8. "John Kasambala, mganga maarufu wa kienyeji wilayani hapa amefariki dunia baada ya kualikwa kwa jirani yake kuweka ndumba kwenye zizi ili lisiingiliwe na wezi wa mifugo" (*Komesha*, Mei 24-30, 2003, uk. 2)

9. "Juma amemwomba 'pilato' Moshi Komba wa mahakama hiyo kumfutia mashitaka yake kutokana na mbuzi aliokwiba kupatikana na kurejeshewa mwenyewe" (*Komesha*, iliyokaririwa, uk. 3)

Tungo nyingi za mada mbalimbali tulizozipitia zinajitokeza katika miundo kama hiyo katika (8) na (9) ambayo kisarufi haionyeshi dosari na inafikisha ujumbe kwa ubora unaotarajiwa. Kisarufi miundo hii ni sanifu na kinachoweza kuitwa cha mitaani ndani mwake inaelekea kuwa ni mada za mitaani na labda maneno ya mitaani kama 'pilato' (maana yake hapa ni 'hakimu').

Lakini hebu tutazame mifano zaidi kutokana na mazingira mengine tofauti ya maelezo. Katika (10) hapa chini tuna mifano ya sentensi kutokana na hadithi fupi ya kubuni:

10.(a) "Alikuwa na begi lake mkononi, akiwa na shauku kubwa ya kumwona kaka yake Rogers ambaye alikuwa hajaonana naye takriban miaka miwili, lakini zaidi ni mke wake, yaani shemeji yake ambaye wakati anaolewa mwaka mmoja uliopita, Tabib hakuhudhuria harusi hiyo zaidi ya kumwona shemejiye kwenye picha." (*Maisha*, Aprili 7-13, 2004, uk. 4)

(b) "Walahi usipoangalia uzalendo utakushinda, mimi nakujua bwana au si weye tuliyekuwa tukikuita Mtabibu wa mapenzi na jina likawa Tabibu na si Tabib tena." (*Maisha*, keshatajwa, msisitizo wangu)

(c) "Shuku alimpachika dongo Tabib ambaye alibaki akitabasamu na kusema 'Hayo yalikuwa ya zamani na yamepita, lakini kubwa ni kwangu kumtamani shemeji yangu? 'Yaani wanawake dunia hii watakuwa wamekwisha hadi nitembee na shem? Sijawahi kufanya hivyo na kamwe sitofanya, ni matusi kwangu kutembea na mtu niliye na mahusiano ya karibu, ninyi mnaweza mimi No'!" (*Maisha*, keshatajwa, msisitizo wangu)

Mifano katika (10) ni ya sentensi ndefu zaidi. Sentensi hizi zimekaririwa kutoka katika hadithi fupi yenye mada ya mitaani isemayo "Shemeji njoo, lakini utaweza?" Kwa maoni yetu, sentensi katika (10a) ni sentensi sanifu kabisa kisarufi na hatuoni kitu tunachoweza kukipambanua kuwa ni cha mitaani. Katika (10b) pia tunakuta sentensi sanifu lakini ambayo imebeba msemo wa mitaani "uzalendo utakushinda" na umbo la neno linalotumika zaidi mitaani "weye". Msemo "uzalendo utakushinda" una maana kuwa utakwama kuendelea na msimamo au matendo yako ya kiadilifu. (10c), kwa upande wake, nayo ni sentensi sanifu isipokuwa kama watumiaji wengine wa lugha watapendelea kuongeza neno "naye" ama baada ya neno "niliye" au baada ya neno "karibu". Hata hivyo, sentensi hii nayo imebeba msemo wa mitaani "pachika dongo" (kusemea maneno yasiyofaa), neno linalofupishwa mitaani "shem" badala ya "shemeji", tungo "sitofanya" linalotumika zaidi mitaani na neno la Kiingereza "No". Katika lugha ya kawaida, wakati sentensi katika (10a) ingebakia hivyo ilivyo, zile katika (10b) na (10c) ingelazimu zirekebishwe kwa kuondoa hivyo vipengele vya mitaani vilivyotajwa na kuweka vile vya kawaida.

Aidha tuliamua kutazama pia tungo katika tahariri za baadhi ya magazeti yenye kipengele hicho. Hebu tuchunguze mifano michache katika (11):

11.(a) "WA...WA...WA...! Mzee wa Buzuki nakufagilia ewe mpendwa msomaji, hususan walengwa wakuu, ambao ni wanamuziki, muweze kupata mwanga kama siyo kufunguliwa macho zaidi katika masuala ya fani hii adhimu" (*Buzuki*, Mei 19-Juni 1, 2003, uk.2)

(b) "Hata hivyo mbali na kuwa kazini kitendo cha kukubali kufa ni ushujaa wa aina yake kwani wako ambao wakiona majambazi wanakimbia au wanatoa siri kwamba watawavizia hivyo wakimbie au wawahi kufanya hujuma zao" (Maisha, Aprili 7-13, 2004, uk. 2)

Katika mifano hii tunaona sentensi ambazo tulitarajia ziwe makini zaidi kisarufi kuliko sentensi tulizokwishakuzitazama hapo juu kwa kuwa ni tahariri. Lakini ni dhahiri kuwa sentensi katika (11a), japokuwa ina vipengele vingi vya kisarufi vya mitaani, bado ina mtiririko mzuri kisarufi kuliko ile katika (11b) ambayo haina vipengele hivyo. Inaonekana sentensi hii katika (11b) ingesomeka vizuri zaidi ingeongezewa tungo "kuwafanya" kati ya maneno "hivyo" na "wakimbie" ili ieleweke vizuri zaidi. Katika (11a) vipengele vya mitaani vilivyopigiwa mistari "WA...WA" inaonyesha kumshangilia mtu kwa alichofanikiwa kukifanya, na "nakufagilia" ina maana ya kufanya mambo yawe mazuri kwako.

4. Hitimisho

Kwa kuvitazama kwa jumla vipengele vya kisarufi kwa maana ya aina za maneno, misemo na tungo mbalimbali katika magazeti ya mitaani, ni dhahiri imeanza kuonekana picha ya lugha ambayo ni mahsusi kwa magazeti haya. Lugha hii kama tulivyoona inafungana sana na lugha inayotumika mitaani hasa jijini Dar es Salaam. Kutokana na urahisi wa mawasiliano baina ya wakazi wa mitaa mbalimbali ya jiji hili, lugha hii imeenea sana katika mitaa mingi wanayoishi raia wa kawaida. Lakini kutokana na magazeti haya kusambazwa katika sehemu nyingi nchini, ni rahisi sasa hivi kuwasikia pia wasemaji katika miji mingine magazeti haya yanakofika, wakitumia maneno na misemo kama hiyo iliyojitokeza katika majadiliano.

Masuala ya kisarufi ya lugha hii yaliyojadiliwa hapa ni yale ya jumla sana. Hii ina maana kuwa bado kunahitajika uchunguzi wa kina kubainisha vipengele vyote muhimu vya lugha hii, mipaka yake ya kijiografia, wahusika na utamaduni wao na mwelekeo au mielekeo ya kukua kwake. Ikifikia hapo ndipo tutaweza kuingiza uchanganuzi unaohusisha vipengele vya mkabala wa Isimuutamaduni tuliougusia katika 3.1. hapo juu. Lakini hata kabla ya hapo, tunafikiri kuwa ni vizuri kuanza kuandaa orodha kamili ya msamiati na misemo ya lugha hii ambayo sasa imepata nguvu kubwa kimaandishi.

5. Marejeo

Blommaert, J. 1990. Standardization and Diversification in Kiswahili: A note on language attitudes. *Kiswahili* 57. Dar es Salaam: TUKI. pp. 22-32.

Krapf, L. 1964 [1850]. *Dictionary of Kisuaheli Language*. Ridgewood: Gregg Press.

Musavi, L. M. 2001. "Magazeti ya Kiswahili na Maendeleo nchini Kenya", katika *Kiswahili: A Tool for Development*, Nairobi: Moi University Press.

Ohly, R. 1982. Report on Lexicographic Research at the Friendship Textile Mill. *Kiswahili* 49/1. Dar es Salaam: TUKI. pp. 78-86.

Palmer, G. B. 1996. *Toward a Theory of Cultural Linguistics.* Austin: University of Texas Press

Magazeti ya Mitaani: *Amani, Buzuki, Cheka, Ijumaa*, *Kasheshe*, *Kombora*, *Komesha*, *Macho*, *Maisha*, *Michapo, Msema Kweli, Nyakati*, *Uwazi*. Matoleo mbalimbali ya mwaka 2003.